Chanjo ya nyongeza aina ya Bivalent ya UVIKO-19

Kuna tofauti gani kati ya nyongeza ya bivalent na za awali?
Chanjo aina ya bivalent ya UVIKO-19 ina sehemu mbili za kutoa kinga bora: sehemu moja ni ya virusi vya awali vya UVIKO-19 na sehemu nyingine ni kwa lahaja ya Omicron.

Ni lini nahitaji kupata nyongeza ya bivalent?
Kila kundi la umri linaweza kuwa na ustahiki tofauti. Makundi yafuatayo yanastahiki muda mfupi kati ya dozi:

- Watu wenye umri wa miaka 70 na zaidi
- Watu wenye umri wa miaka 12 na zaidi ambao wana kinga dhaifu kiasi au sana
- Watu wenye umri wa miaka 12 na zaidi ambao ni wakazi wa sehemu za kutunzia watu kwa muda mrefu au sehemu ambazo wazee wanaishi
- Watu wenye umri wa miaka 55 na zaidi ambao ni Mataifa ya Kwanza
- Watu wenye umri wa miaka 50 na zaidi ambao ni WaNova Scotia wenye asili ya Kiafrika
- Wajawazito

Kwa mapendekezo yaliyo sasishwa, angalia https://www.nshealth.ca/coronavirusvaccine. Kama una maswali tafadhali piga simu: 1-833-797-7772 (Jumatatu hadi Ijumaa, saa 1 asubuhi hadi saa 1 jioni na Jumamosi hadi Jumapili, saa 4 asubuhi hadi saa 12 jioni). Huduma za Ukalimani hutolewa unapopiga namba hii.

Je, wajawazito au wanaonyonyesha wanapaswa kupata chanjo ya nyongeza aina ya bivalent?
Ndiyo. Afya ya umma inapendekeza sana kwamba watu wanaopanga kupata mimba, au ni wajawazito au wanaonyonyesha, wapate chanjo zao za UVIKO-19. Kama ilivyoelezwa hapo juu, wajawazito wanastahili muda mfupi kati ya chanjo.

Ikiwa tayari nilikuwa na Uviko, ni lini ninapaswa kupata nyongeza ya bivalent?
Inategemea kama umepata mfululizo wako wa msingi wa chanjo au la. Tafadhali rejea sehemu: " Ustahiki wa Chanjo Baada ya Kupona UVIKO-19" kwenye tovuti hii: https://www.nshealth.ca/coronavirusvaccine.

Je, ninaweza kupata chanjo ya mafua na nyongeza ya UVIKO-19 kwa wakati mmoja?
Ndiyo. Watu wenye umri wa miaka 5 na zaidi wanaweza kupata chanjo ya mafua kwa usalama kabla, baada au hata wakati huo huo wa kupata nyongeza. Hii inaweza kubadilika na kujumuisha watoto wadogo. Kwa maelezo zaidi, angalia https://novascotia.ca/flu/?gclid=EAIaIQobChMI-4uuzdrE_AIVDTizAB3VMg1JEAAYASAAEgJYyfD_BwE

Je, watoto wangu wanaweza kupata chanjo nyingine za watoto na nyongeza ya UVIKO-19 kwa wakati mmoja?
Inategemea. Zungumza na mtaalamu wa afya kubaini muda wa chanjo za UVIKO-19 na chanjo zisizo za UVIKO-19.

Je, ni salama kiasi gani kupata chanjo ya Uviko-19?
Baada ya kuchanjwa, ni kawaida kuwa na madhara ya muda. Haya kwa kawaida hudumu kutoka saa chache hadi siku chache baada ya chanjo. Madhara ya kawaida ni pamoja na wekundu, uvimbe na/au maumivu kwenye sehemu uliyochomwa sindano. Kunaweza kuwa na madhara zaidi ya jumla kama vile uchovu, baridi, homa kiasi, maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli na maumivu ya viungo. Huu ni mwitikio wa asili wa mwili kujenga kinga.

Kuna uwezekano mdogo wa mzio mkubwa kwa chanjo inayoitwa anaphylaxis. Kwa kawaida hutokea muda mfupi baada ya mtu kupewa chanjo na mzio huo unatibika. Ndiyo maana utatakiwa kukaa kliniki kwa muda usiopungua dakika 15 baada ya chanjo ili wafanyakazi waweze kuangalia athari hizi adimu sana na kuzitibu haraka. Kwa taarifa zaidi juu ya madhara, angalia https://www.nshealth.ca/coronavirus-what-expect-covid-19-vaccine-clinic

Ikiwa nimepata chanjo ya Uviko- 19 katika nchi nyingine, je, nipate nyongeza ya bivalent?
Ndiyo. Walakini, rekodi zako za chanjo lazima ziwe kamili na ziingizwe katika mfumo wa afya wa Nova Scotia kabla ya kuweka miadi yako ya kupata nyongeza.

isans Immigrant Services Association of Nova Scotia

Unaweza kupakia uthibitisho wako wa chanjo kutoka nchi nyingine au mkoa mwingine kupitia kiungo hiki: https://vaccineentryservice.novascotia.ca/ . Rekodi zako zinaweza kuchukua wiki chache kusasishwa.

Je, ninapataje uthibitisho wangu wa chanjo?
Unaweza kupata uthibitisho wako wa chanjo hapa: https://novascotia.flow.canimmunize.ca/en/portal . Tafadhali kumbuka kuwa dozi zako za awali katika nchi nyingine hazionekani moja kwa moja katika mfumo huu hadi utakapozipakia, kama ilivyoelezwa katika swali lililopita.

Ninawezaje kupata nyongeza ya bivalent?
Kabla ya kuanza:

- Unahitaji kadi halali ya afya ya Nova Scotia ili kuweka miadi mtandaoni.
- Kama **huna** kadi ya afya, piga simu 1-833-797-7772. Huduma za ukalimani zinapatikana.
- Ikiwa unataka dozi ya ziada au ya nyongeza ya chanjo ya UVIKO-19, unaweza kuhitajika kuonyesha uthibitisho wa kustahiki. Hii inamaanisha chanjo zako za awali za UVIKO-19 zinahitaji kusasishwa katika mfumo wa Nova Scotia. Ili kupakia dozi zako ulizopata katika nchi nyingine au mkoa, nenda kwenye tovuti hii: https://vaccineentryservice.novascotia.ca/

Jinsi ya Kuweka Miadi:

- Mtandaoni kwa kliniki: https://novascotia.flow.canimmunize.ca/en/covid-flu-booking
- Piga simu 1-833-797-7772 (Jumatatu hadi Ijumaa, saa 1 asubuhi hadi saa 1 jioni na Jumamosi hadi Jumapili, saa 4 asubuhi hadi saa 12 jioni).
    - Ikiwa unahitaji ukalimani, piga namba hii ili uweke miadi (zaidi ya lugha 125 tofauti zinapatikana).
- Unapopiga namba hii, mtaalamu atapitia maswali ya uchunguzi wa afya pamoja na wewe na kujibu wasiwasi wako kuhusu chanjo.
- Kwa habari zaidi, angalia ISANS's Jinsi ya Kuweka Miadi ya Chanjo - Tovuti ya Mradi wa Beacon .

Jinsi ya kupata kliniki ya kuingia bila miadi

- Chanjo pia hutolewa katika kliniki mbalimbali za kuingia bila miadi. Maeneo na nyakati hizi hubadilika wiki hadi wiki. https://www.nshealth.ca/drop-in-vaccine-clinics
- Maduka ya dawa pia hutoa kliniki za bila miadi:
- Maduka ya dawa pia yanaweza kutoa vipeperushi kwa lugha tofauti wakati wateja wanapopata chanjo zao.